# Utafiti wa viashirio vya UKIMWI



## Tanzania Bara 2003-04

## MATOKEO MUHIMU

Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Mpango wa kudhibiti UKIMWI Tanzania

Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania

**MASAHIHISHO**

**Ukurasa wa 10**

i) Makosa katika 'Ufunguo' wa mchoro; inaposomeka 'Wanaume' inatakiwa isomeke 'Wanawake', na kinyume chake.

ii) Maelezo 'asilimia 17 ya wavulana na asilimia 26 ya wasichana' yanatakiwa yawe 'asilimia 17 ya wasichana na asilimia 27 ya wavulana'.

**Ukurasa wa 11 na 12**

Makosa katika 'Ufunguo' wa mchoro; inaposomeka 'Wanaume' inatakiwa isomeke 'Wanawake', na kinyume chake.

**Ukurasa wa 14**

Kichwa cha habari cha mchoro kinatakiwa kusomeka 'Asilimia ya wanawake na wanaume ............ kwa umri kamili walipoingia katika ndoa kwa mara ya kwanza'.

kubuni mikakati mipya katika kupambana na maradhi haya.

Kabla ya utafiti huu, makadirio ya kiwango cha maambukizo ya UKIMWI kitaifa yalitegemea watu wanaojitolea damu kwa ajili ya watu wengine, pia akina mama wajawazito waliokwenda kupata huduma za kliniki wakati wa ujauzito wao. Japokuwa taarifa kutoka katika makundi haya zimekuwa na umuhimu katika kufuatilia mwenendo wa hali ya Virusi katika Tanzania, kujumuishwa upimaji wa virusi vya UKIMWI katika utafiti huu kunatoa nafasi nzuri zaidi katika kufahamu ukubwa na mwenendo wa maambukizo kwa watu walio katika umri wa kuweza kuzaa katika Tanzania. Matokeo ya utafiti huu pia yanatarajiwa kuboresha makisio ya kila mwaka ya kiwango cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI kabla ya kufanyika utafiti mwingine wa aina hii.

Ripoti hii ni muhtasari wa matokeo ya utafiti wa Viashirio vya Afya uliofanyika katika kaya zilizotembelewa mwaka 2003-04. Utafiti huu ulitayarishwa ili kutoa kiwango cha maambukizo ya Virusi Vya UKIMWI kimkoa katika Tanzania Bara. Maelezo, picha, pamoja na michoro iliyomo katika ripoti hii vinalenga katika kutoa picha kwa muhtasari wa viashirio muhimu vya UKIMWI ili kuwawezesha watunga sera na wapanga mipango wanaohitaji takwimu za wakati uliopo kwa ajili kutathmini utendaji wao na mwelekeo katika siku zijazo.

Meja Jenerali (Mstaafu) Herman C. Lupogo
Mwenyekiti Mtendaji
Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania
Dar Es Salaam

Cletus P.B. Mkai
Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Dar Es Salaam

# UTANGULIZI

Utafiti wa viashiria vya UKIMWI Tanzania Bara 2003 – 04 ni wa kwanza unaohusu kaya binafsi kufanyika tangu walipogunduliwa wagonjwa watatu wa kwanza wa UKIMWI mwaka 1983. Dodoso binafsi lilitumika kukusanya taarifa za kina kutoka kwa wanawake na wanaume wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 49 waliokutwa katika kaya zilizochaguliwa kitaalam nchini kote Tanzania Bara ambapo jumla ya kaya 6,901 zilifanyiwa utafiti kuanzia mwezi Desemba 2003 hadi mwisho wa Machi 2004. Wanawake wapatao 7,154 na wanaume wapatao 6,196 walistahili kwa mahojiano binafsi, ambapo wanawake 6,863 na wanaume 5,659 walihojiwa.

Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kuwawezesha wapanga mipango pamoja na watunga sera wanaojihusisha na UKIMWI kuwa na taarifa zinazohitajika katika kupanga na kutekeleza mipango mbali mbali pamoja na kutafuta na kugawanya rasilimali kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini mipango iliyopo na kubuni mikakati mipya kwa ajili ya kupambana na maradhi haya.

Maeneo 345 ya kuhesabia yaliyotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 yalichaguliwa kitaalam ambapo kaya 20 zilichaguliwa katika kila eneo kwa ajili ya mahojiano ya dodoso la kaya na la binafsi. Kazi ya ukusanyaji takwimu ilihusisha uchukuaji wa sampuli ya damu kwa ajili ya kupima maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Kwa ujumla, wakusanyaji wa takwimu hizi walikuwa ni wauguzi 75 kutoka Wizara ya Afya. Takwimu zilizokusanywa zilihusu masuala ya kijamii, kiuchumi pamoja na taarifa za watu zikiwemo ufahamu, mwenendo, matendo, na tabia juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Matone ya damu yalichukuliwa kwa kutumia karatasi maalum (filter paper) kutoka kwa mhojiwa aliyekubali kwa hiari yake. Uchunguzi wa matone ya damu ulifanyika katika maabara ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi na Tiba katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.



Asilimia 99 ya kaya zote zilihojiwa, wakiwemo asilimia 96 ya wanawake na asilimia 91 ya wanaume. Waliohojiwa katika maeneo ya vijijini walikuwa wengi zaidi ikilinganishwa na maeneo ya mijini. Sababu kubwa iliyochangia ni kutowapata katika kaya zao licha ya kuwarudia mara kadhaa.

## HALI YA KAYA, MAKAZI PAMOJA NA WAHOJIWA

Tanzania ina idadi kubwa ya watu katika umri mdogo wa chini ya miaka 24. Wengi wa wakuu wa kaya katika maeneo ya mijini na vijijini ni wanaume.


Utafiti unaonesha kuwa wastani wa kila kaya ni watu 5. Watoto wapatao asilimia 60 wenye umri wa chini ya miaka 18 wanaishi na wazazi wao halisi wakati wale wasioishi na wazazi halisi, hata mmoja ingawa wazazi wote wako hai wanafikia asilimia 11.

**Kiwango cha Elimu cha Wanakaya**

Utafiti umebaini kuwa asilimia 20 ya wanaume wenye umri kati ya miaka 6 na kuendelea hawana kiwango chochote cha elimu wakati wanawake ni asilimia 29. Wanaume walio na elimu kiasi fulani ni asilimia 40 wakati wanawake ni asilimia 35. Kwa ujumla, kiwango cha wanawake na wanaume walio na elimu ni kikubwa mijini ikilinganishwa na vijijini.

**Hali ya Makazi**

Matokeo yanaonesha uduni wa hali ya vijijini kuhusiana na umeme, maji ya kunywa, aina ya paa za nyumba zinamoishi kaya, sakafu, nishati ya kupikia na ile ya kuangazia ndani. Asilimia 11 ya kaya katika Tanzania Bara ndizo zenye umeme, na kwa upande wa maji ni asilimia 79 ya kaya zinazoishi mijini zinapata maji salama, na asilimia 43 ya kaya za vijijini zinapata maji salama. Nyumba nyingi za vijijini zimeezekwa kwa nyasi na udongo (asilimia 62). Asilimia 65 ya kaya za mijini hutumia mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia, wakati nyingi ya kaya za vijijini zinatumia kuni.



Baadhi ya rasilimali za kudumu katika kaya zilizingatiwa kama vitu muhimu katika utafiti huu kwa ajili ya kuangalia hali ya umaskini katika kaya. Rasilimali hizi zinajumuisha gari/lori, pasi (ya umeme au ya mkaa), seti ya televisheni, simu, jokofu, baiskeli, pikipiki, akaunti ya akiba benki, n.k. Asilimia 31 ya kaya katika Tanzania Bara hazimiliki hata moja ya rasilimali hizi, na nyingi ya kaya hizi ni za vijijini (asilimia 36) na mijini ni asilimia 18.


# UFAHAMU WA VIRUSI VYA UKIMWI NA UGONJWA WA UKIMWI

Njia kuu ya kuenea kwa virusi vya UKIMWI ni ngono baina ya watu wa jinsi mbili tofauti, njia hii huchangia hadi asilimia 90 ya maambukizo yote katika Tanzania Bara (Ofisi ya Waziri Mkuu, Novemba 2001), ikifuatiwa na ile ya maambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Mtoto huambukizwa akiwa tumboni, au wakati wa kuzaliwa, au wakati wa kunyonya. Njia nyingine ni kuongezewa damu yenye virusi au kuwekewa viungo vya mwili kutoka kwa mtu ambaye ameathirika.

**Ufahamu wa Ugonjwa wa UKIMWI**

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa zaidi ya asilimia 99 ya watu wote wa Tanzania Bara wenye umri wa miaka kati ya 15 – 49 wamewahi kusikia juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Ufahamu wa UKIMWI ni mkubwa ukiwa ni asilimia 96 ya waliohojiwa katika rika zote, mikoa yote, mijini na vijijini, wenye viwango tofauti vya elimu. Kwa jumla idadi ya watu waliowahi kusikia juu ya UKIMWI imeongezeka kiasi kati ya mwaka 1999 na sasa.

Matokeo yanaonesha kwamba ufahamu juu ya njia za kujikinga na UKIMWI umeongezeka sana. Zaidi ya watu wanne katika kila watu watano (asilimia 87 ya wanawake na asilimia 88 ya wanaume) walionesha kwamba uwezekano wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI unaweza kupungua kwa kuwa na mpenzi mmoja tu ambaye hajaambukizwa na ambaye hana wapenzi wengine. Asilimia 68 ya wanawake na asilimia 75 ya wanaume walisema watu wanaweza kupunguza uwezekano wao wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI ikiwa watatumia mpira (kondomu) kila mara wafanyapo tendo la kujamiiana. Ufahamu wa njia zote hizi za kujikinga na maambukizo ya virusi vya UKIMWI ni mkubwa, ikiwa ni asilimia 63 ya wanawake na asilimia 69 ya wanaume wameonesha njia zote za kupunguza hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Kama ilivyotarajiwa, idadi ya wanawake na wanaume wanaofahamu kwamba kusubiri au kutofanya kabisa ngono kunapunguza uwezekano wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI ni asilimia 87. Ulinganifu baina ya wanawake na wanaume juu ya uelewa unatofautiana, wanaume wana uelewa zaidi ya wanawake.




## Ufahamu wa Maambukizo ya UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto

Katika kila wanawake 10 karibu wanawake 7 (asilimia 69) na zaidi ya wanaume 6 katika kila wanaume kumi (asilimia 63) wanafahamu kwamba mtoto mchanga anaweza kuambukizwa virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwa njia ya kunyonya. Ufahamu wa dawa maalum za kupunguza makali ya UKIMWI bado ni mdogo; asilimia 17 ya wanawake na 19 ya wanaume wanafahamu kwamba daktari au muuguzi anaweza kumpatia mama mjamzito ambaye ana virusi vya UKIMWI dawa maalum za kumwepusha mtoto atakayezaliwa kupata maambukizo. Halikadhalika asilimia 15 ya wanaume na wanawake wanafahamu kwamba mtoto mchanga anaweza kuambukizwa virusi kwa njia ya kunyonya na kwamba hatari hii inaweza kupunguzwa kwa matumizi ya dawa hizo maalum.



## Kukataliwa kwa imani potofu juu ya Maambukizo ya Ugonjwa wa UKIMWI

Kumekuwa na ongezeko kubwa katika kiwango cha ufahamu wa msingi juu ya virusi vya UKIMWI katika kipindi cha miaka 5 iliyopita Tanzania Bara. Idadi ya wanawake wanaofahamu kwamba mtu anayeonekana kuwa mwenye afya njema anaweza kuwa na virusi vya UKIMWI imeongezeka kutoka asilimia 69 ya mwaka 1999 hadi asilimia 78 katika utafiti huu, na kutoka asilimia 77 hadi 84 ya wanaume. Halikadhalika idadi ya wanawake wanaojua kwamba UKIMWI hauambukizwi kwa kuumwa na wadudu imeongezeka kutoka asilimia 54 mwaka 1999 hadi asilimia 71 katika utafiti huu, na idadi ya wanawake wanaosema mtu hawezi kuambukizwa virusi kwa kula kwenye sahani moja na mtu mwenye virusi vya UKIMWI imeongezeka kutoka asilimia 58 hadi 76.



# MTAZAMO KUHUSIANA NA VIRUSI NA UGONJWA WA UKIMWI


## Unyanyapaa kuhusiana na Ugonjwa wa UKIMWI

Katika utafiti huu, wahojiwa waliosema wamewahi kusikia juu ya ugonjwa wa UKIMWI waliulizwa maswali kadhaa yaliyohusiana na mtazamo wao kwa watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI. Utafiti umeonesha kwamba katika kila watanzania 10, 9 wako tayari kuwatunza ndugu wanaougua UKIMWI katika kaya zao. Hata hivyo wanawake wachache (asilimia 52) wakilinganishwa na wanaume (asilimia 63) walionesha kuwa tayari kununua aina mbali mbali za mboga za majani kutoka kwa muuzaji ambaye anafahamika kuwa anaugua au ana virusi vya UKIMWI.

Watanzania wapatao 7 kati ya 10 wanasema mwalimu wa kike ambaye ana virusi vya UKIMWI lakini haumwi, anaweza kuendelea kufundisha. Wanawake 6 kati ya 10 na wanaume 7 kati ya 10 wanasema kwamba ikiwa mmoja wa wanafamilia atakuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI, hawataliona kuwa ni jambo la siri. Kwa ujumla utafiti huu umeonesha watanzania walio wengi hawawanyanyapai watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wanaougua UKIMWI.

## Mtazamo katika kujadiliana juu ya ngono salama

Utafiti unaonesha kwamba watanzania 8 kati ya 10 wanaafiki kwamba mke anayo haki ya kukataa kufanya ngono na mume wake ikiwa atagundua kwamba mumewe ana ugonjwa wa zinaa, wakati wanawake 7 kati ya 10 na wanaume 8 kati ya 10 wanaamini kwamba mke anayo haki ya kumtaka mumewe kutumia kondomu ikiwa atagundua mumewe ana ugonjwa wa zinaa.



**Mtazamo kuhusiana na kufundisha watoto wa umri wa miaka 12 – 14 juu ya matumizi ya kondomu**

Utafiti umeonesha kuwa watanzania 6 kati ya 10 wanaunga mkono ufundishwaji wa matumizi ya kondomu kwa watoto wa umri wa miaka 12 hadi 14. Hata hivyo watanzania wengi wa umri wa miaka 40-49 hawaungi mkono wazo hili ikilinganishwa na wale walio katika umri wa chini.

# TABIA ZINAZOCHANGIA MAAMBUKIZO YA VIRUSI VYA UKIMWI

## Wapenzi zaidi ya mmoja

Utafiti umeonesha kwamba asilimia 6 ya wanawake na asilimia 27 ya wanaume waliofanya tendo la kujamiiana katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, walijihusisha na tendo hilo na wapenzi zaidi ya mmoja. Idadi yao inatofautiana baina ya wanaume ambao wameoa au wamewahi kuoa na wale ambao hawajawahi kuoa. Asilimia 10 ya wanawake ambao hawajawahi kuolewa walieleza kufanya ngono na wapenzi angalau wawili tofauti katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti ikilinganishwa na asilimia 6 ya wale walioolewa au kuwahi kuolewa. Theluthi moja ya wanaume ambao hawajawahi kuoa walisema wamekuwa na zaidi ya mpenzi mmoja ikilinganishwa na mwanaume mmoja katika kila wanne waliooa ambao wamekuwa na mpenzi zaidi ya mmoja katika kipindi cha miezi 12 kabla ya siku ya utafiti.




## Ngono hatari na kufanya ngono na makahaba

Katika utafiti huu, ngono hatari ilichukuliwa kuwa ni tendo la kufanya ngono na mtu ambaye si mwenza wa kawaida. Utafiti huu umebaini kuwa asilimia 23 ya wanawake na asilimia 46 ya wanaume waliofanya ngono katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, walijihusisha na ngono hatari. Wanawake 4 katika kila wanawake 10 (asilimia 38) na nusu ya wanaume (asilimia 50) walieleza kutumia kondomu wakati wa kufanya ngono hatari. Hii inaonesha kuwa wanawake wako nyuma katika matumizi ya kondomu wakati wa kufanya ngono na watu ambao si wenza wao wa kawaida.


Katika kundi hili la watu wanaofanya ngono hatari wanapatikana makahaba., Katika wanaume waliohojiwa, ni wanaume wawili kati ya wanaume 100 (asilimia 2) ndio waliojihusisha katika kufanya ngono na makahaba miezi 12 kabla ya utafiti. Na wengi wa wanaume hawa waliofanya ngono na makahaba, walitumia kondomu katika tendo la hivi karibuni (asilimia 58).

## Ushauri Nasaha na Kupima Virusi kwa Hiari

Ushauri nasaha pamoja na kupima kwa hiari virusi vya UKIMWI ni hatua muhimu. Hii inamwezesha mtu kufahamu namna ya kuweza kuishi kwa muda mrefu akiwa na virusi vya ugonjwa huu au namna ya kuepuka maambukizo ya virusi ikiwa hajaambukizwa na bado anajihusisha na matendo ya kujamiiana. Idadi ya wale ambao walisema wamewahi kupima afya zao ili kufahamu kama wameambukizwa virusi vya UKIMWI au bado inalingana kwa wanaume na wanawake. Asilimia 5 ya wanawake na asilimia 7 ya wanaume walipimwa na kupewa majibu ya vipimo vyao katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti.


Idadi ya watu waliopima kufahamu hali ya afya zao inaonekana kwa kiasi kikubwa kuwa na uhusiano na kiwango cha elimu cha mhusika. Imeonekana kadiri kiwango cha elimu kinavyoongezeka ndivyo mtu anavyokuwa tayari zaidi kutaka kufahamu hali ya afya yake kama ameambukizwa virusi vya UKIMWI ama bado. Hali hii imejionesha kwa wanaume na wanawake wote waliohojiwa katika utafiti huu.

**Asilimia ya wanawake na wanaume waliopima virusi vya ukimwi na kupokea majibu ya vipimo kwa hali ya kiuchumi**




## Kiwango cha maambukizo ya magonjwa ya ngono

Maambukizo ya magonjwa ya ngono yana uhusiano wa moja kwa moja na maambukizo ya virusi vya UKIMWI. Pia utafiti huu umegundua kwamba wanaume ni rahisi zaidi kuripoti kuwa na magonjwa ya zinaa kuliko wanawake. Hii inawezekana kutokana na tofauti za maumbile, ambayo uambukizi kwa wanaume ni rahisi kuhisi au kuona dalili kuliko wanawake.




## Ukeketaji Wanawake na Tohara kwa Wanaume

Ukeketaji pamoja na zoezi zima la tohara za jadi humweka mhusika (yaani mwenye kukeketwa au kutahiriwa) katika hatari kubwa ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI ikiwa mazingira pamoja na vifaa vitumiwavyo kwa ujumla siyo safi na salama. Utafiti umeonesha kuwa utamaduni wa ukeketaji wanawake kwa baadhi kwa baadhi ya sehemu katika Tanzania bado upo licha ya serikali kuupiga marufuku.

# MATOKEO YA UTAFITI KUHUSIANA NA VIJANA

## Uyatima

Uyatima unaelezwa kuwa ni ile hali ya mtoto wa umri wa chini ya miaka 18 kufiwa aidha na mzazi mmoja au wazazi wote wawili. Ikumbukwe katika Tanzania, mtoto ni yule mwenye umri wa chini ya miaka 18. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba asilimia 11 ya watoto wote wamefiwa na aidha mzazi mmoja au wazazi wote wawili. Matokeo haya yanaonesha asilimia 4 ya watoto walio na umri chini ya miaka 18 wamefiwa na mama zao halisi, asilimia 8 wamefiwa na baba zao halisi na asilimia 1 wamepoteza wazazi wote wawili. Kwa ujumla, yatima ni wengi katika maeneo ya mijini (asilimia 14) kuliko katika maeneo ya vijijini (asilimia 10).




## Tendo la ngono kwa mara ya kwanza

Umri ambao watu huanza kufanya tendo la kujamiiana una umuhimu wa pekee kutokana na ukweli kwamba virusi vya UKIMWI huenea kwa kiasi kikubwa sana kwa njia hii ya kujamiiana baina ya mwanaume na mwanamke. Asilimia 11 ya wasichana wenye umri wa miaka kati 15 hadi 24 wamegundulika kuwa walifanya tendo hili kwa mara ya kwanza wakiwa na umri wa miaka 15 ikilinganishwa na asilimia 10 ya wavulana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 ambao walifanya tendo la kujamiiana wakiwa na umri wa miaka 15. Kwa ujumla wanawake wanaonekana kuanza kufanya tendo la ngono katika umri mdogo zaidi ikilinganishwa na wanaume.

## Matumizi ya kondomu kwa tendo la kwanza la kujamiiana baina ya vijana

Pamoja na kuchelewa kuanza kujihusisha katika kufanya tendo la ndoa, matumizi ya kondomu ya kila mara ni njia ya kuwaepusha vijana kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Kati ya wavulana na wasichana wenye umri wa miaka kati ya 15 na 24 waliosema wamewahi kujamiiana, asilimia 17 ya wavulana na asilimia 26 ya wasichana walitumia kondomu walipofanya tendo hili kwa mara yao ya kwanza. Utafiti pia umegundua kuwepo kwa uhusiano mkubwa wa kiwango cha elimu na utumiaji wa kondomu kwa tendo



la mara ya kwanza. Asilimia 49 ya wasichana wenye elimu ya sekondari na zaidi walitumia kondomu walipofanya tendo la ngono kwa mara ya kwanza ikilinganishwa na asilimia 8 tu ya wasichana waliotumia kondomu ambao hawana elimu yoyote. Kwa jumla, matumizi ya kondomu yanaonekana kuongezeka kwa kadri mtu anavyokuwa na kiwango kikubwa cha elimu katika Tanzania Bara.


### Tendo la kujamiiana kabla ya ndoa

Kipindi kati ya kujamiiana kwa mara ya kwanza na kuolewa au kuoa, kwa kawaida vijana hukichukulia kama ni kipindi cha kufanya majaribio. Kwa hali ya sasa ya ugonjwa huu wa UKIMWI, tabia hii inaweza kuwa ya hatari. Katika kila wasichana 10 ambao hawajawahi kuolewa, 6 walisema hawajawahi kufanya tendo la kujamiiana ikilinganishwa na wavulana ambao ni chini ya nusu (asilimia 46) wa umri wa kati ya miaka 15 hadi 24 ambao walisema hawajawahi kufanya tendo la kujamiiana. Kwa upande wa elimu, imeonekana kwamba vijana ambao hawakumaliza elimu ya msingi na ambao hawajaolewa au kuoa, hawakujihusisha kwa kiasi kikubwa na tendo la kujamiiana katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti.

### Ngono hatari na matumizi ya kondomu


Njia iliyo kuu ya kuenea kwa virusi vya UKIMWI, ni kwa kujamiiana kati ya mwanamke na mwanaume bila kuchukua tahadhari wakati mmoja wao akiwa ameshaambukizwa. Kuepuka maambukizo ya virusi vya UKIMWI, ni muhimu kuchukua tahadhari kwa; kusubiri, au kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja ambaye hajaambukizwa. Ikishindikana njia mojawapo katika hizi, basi ni vema kutumia kondomu kila mara lifanyikapo tendo la kujamiiana.

Vijana wa umri wa kati ya miaka 15 hadi 24 waliosema walijihusisha na tendo la kujamiiana katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, asilimia 37 ya wasichana na asilimia 81 ya wavulana walijihusisha na ngono hatari (ngono bila kutumia kondomu). Kwa ujumla ngono hatari kwa vijana inaonekana kupungua kadri kiwango cha elimu kinavyoongezeka.



## Ufahamu wa Mahali zinakopatikana Kondomu

Ufahamu wa vijana juu ya mahali zinakopatikana kondomu, vijana waishio mijini wanafahamu zaidi ikilinganishwa na vijana waishio vijijini katika Tanzania Bara.




Ufahamu huu unaongezeka kwa kadri kiwango cha elimu kinavyoongezeka. Ufahamu wa wavulana juu ya mahali zinakopatikana kondomu umeongezeka kutoka asilimia 61 ya wale wasio na elimu hadi asilimia 90 ya wale wenye elimu ya sekondari na zaidi.

## Msaada kwa Kaya zenye watu wazima ambao ni Wagonjwa wa muda mrefu


Kati ya wanaume na wanawake wenye umri wa miaka 18 hadi 59 ambao wamekuwa wagonjwa wa muda mrefu (wagonjwa sana kwa muda wa angalau miezi 3 au zaidi katika miezi 12 kabla ya utafiti), asilimia 16 walisema kaya zao zimepokea aina fulani ya matibabu ya bure katika mwaka uliotangulia kabla ya utafiti. Kwa upande mwingine asilimia 14 walipata msaada wa ushauri na asilimia 12 walipata msaada wa vitu au kusaidiwa kufanya shughuli mbali mbali. Hata hivyo, misaada hii ya aina tatu, inaonekana kuzinufaisha zaidi kaya za mijini kuliko za vijijini, pia kaya zenye hali nzuri kiuchumi.

# NDOA NA TENDO LA KUJAMIIANA

## Hali ya Sasa ya Ndoa

Asilimia 24 ya wanawake wa umri kati ya miaka 15 hadi 49 hawajawahi kuolewa, asilimia 64 wanaishi katika ndoa na asilimia 12 waliwahi kuishi katika ndoa lakini hawapo katika ndoa kwa sasa.

**Asilimia ya wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15 – 49 kwa hali ya ndoa**





Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba idadi ya wanawake ambao hawajawahi kuolewa inapungua kadri umri unavyoongezeka, wakati ambapo idadi ya waliowahi kuishi katika ndoa lakini kwa sasa hawapo katika ndoa inaongezeka kadri umri unavyoongezeka. Takwimu hizi zikilinganishwa; idadi kubwa ya wanaume hawajawahi kuoa, na idadi ndogo aidha wameoa au waliwahi kuwa na ndoa lakini hawapo katika ndoa kwa sasa.

## Ndoa za Wake Wengi

Utafiti unaonesha kwamba mwanamke mmoja katika kila wanawake kumi walioolewa anaishi katika ndoa ya mke zaidi ya mmoja (ana wake wenza mmoja au zaidi) na wanawake wenye umri mkubwa zaidi ndio wanaonekana kwa kiasi kikubwa kuwa katika ndoa za aina hii. Ndoa za namna hii zimeonekana kuwa za kawaida hasa katika maeneo ya vijijini kuliko ya mijini.

**Asilimia ya wanawake na wanaume wanaoishi katika ndoa za mke zaidi ya mmoja kwa sasa kwa umri**





Kama ilivyo kwa wanawake, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba mwanaume mmoja katika kila wanaume kumi ana wake zaidi ya mmoja.

## Umri wa kuingia katika Ndoa kwa mara ya kwanza

Matokeo yanaonesha kwamba mwanamke mmoja katika kila wanawake kumi (asilimia 10) wenye umri kati ya miaka 20 hadi 49 aliolewa kabla ya kutimiza umri wa miaka 15; na karibu theluthi 2 (asilimia 62) ya wanawake wote huingia katika maisha ya ndoa kabla ya kutimiza umri wa miaka 20. Kwa wastani wanawake walio wengi wanaolewa wakiwa na umri wa miaka 19. Asilimia 16 ya wanaume wenye umri wa miaka 20 hadi 49 walioa kabla ya kutimiza umri wa miaka 20, na karibu nusu walioa kabla ya kutimiza umri wa miaka 25 wakati wastani wa umri wa wanaume kuoa ikiwa ni miaka 25.

**Asilimia ya wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 20-49 kwa umri kamili walipojamiiana kwa mara ya kwanza**




## Umri wa Tendo la Kujamiiana kwa Mara ya Kwanza

Asilimia 12 ya wanawake wenye umri wa miaka kati ya 20 hadi 49 walifanya tendo la kujamiiana kabla ya kufikisha umri wa miaka 15, wakati zaidi ya nusu walikuwa wameshajamiiana hadi kufikia umri wa miaka 18. Utafiti unaonesha kuwa wanawake wenye umri mkubwa wanakuwa wazi zaidi kueleza kama walifanya tendo la kujamiiana walipokuwa wadogo. Wanawake wenye umri chini ya miaka 40 wanaonekana kuwa walijamiiana kwa mara ya kwanza wakiwa na umri wa miaka 18. Wanawake wenye umri wa zaidi ya miaka 40 waliripoti wastani wa miaka 17 walipojamiiana kwa mara ya kwanza. Kwa upande wa wanaume, asilimia 7 walisema walijamiiana kwa mara ya kwanza kabla ya kutimiza umri wa miaka 15. Kwa wastani, wanaume wameonekana kuanza kujamiiana wakiwa na umri wa miaka 19.

# KIWANGO CHA MAAMBUKIZO YA VIRUSI VYA UKIMWI

## Kiwango cha Maambukizo ya Virusi vya UKIMWI Kwa Umri na Jinsia


Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba watanzania 7 katika kila watanzania 100 wameambukizwa virusi vinavyosababisha UKIMWI. Idadi ya wanawake walioambukizwa virusi ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya wanaume; ambapo wanawake walioambukizwa ni asilimia 8 na wanaume ni asilimia 6.

Wanawake wengi wanaonekana kuathirika na virusi katika umri mdogo ikilinganishwa na wanaume, isipokuwa katika umri wa miaka 15 hadi 19 ambapo maambukizo ni asilimia 2 kwa wanawake na wanaume. Maambukizo ni ya kiwango kikubwa zaidi kati ya wanawake wenye umri wa miaka 20 hadi 39 ikilinganishwa na wanaume walio katika umri kama huo.

Kiwango cha maambukizo ni kikubwa zaidi kwa wanaume wa umri wa miaka 40 hadi 49 ikilinganishwa na wanawake wenye umri kama huo.

## Kiwango cha Maambukizo ya Virusi vya UKIMWI Kimkoa

Utafiti unaonesha kwamba asilimia 11 ya waathirika wa virusi vya UKIMWI wanaishi mijini




ikilinganishwa na asilimia 5 ya waathirika ambao wanaishi vijijini kwa jinsia zote.

Mikoa iliyo na kiwango cha juu cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI inajumuisha Mbeya, Iringa, na Dar Es Salaam. Mikoa yenye kiwango cha chini cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI ni Manyara na Kigoma.

## Kiwango cha maambukizo kwa vigezo vingine

Utafiti unaonesha kwamba wale wote waliosema wamewahi kuoa au kuolewa lakini wakati wa utafiti walikuwa hawaishi katika ndoa, wameonekana kuwa na kiwango cha juu cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI (asilimia 18) ikilinganishwa na wale ambao kwa sasa wanaishi katika ndoa (asilimia 7 wameambukizwa) au ambao hawajawahi kuoa au kuolewa wameambukizwa kwa asilimia 3. Wahojiwa waliokutwa katika ndoa za wake zaidi ya

mmoja, wameonekana kuwa katika nafasi kubwa ya kuathirika na virusi vya UKIMWI ikilinganishwa na wale ambao wako katika ndoa ya mke mmoja.

Wanawake wanane katika kila wanawake 100 ambao wakati wa utafiti hawakuwa wajawazito wameambukizwa virusi vya UKIMWI wakati wanawake 7 katika kila 100 waliokuwa wajawazito, ni waathirika wa virusi vya UKIMWI.

Wanawake waliosema wamejihusisha na ngono hatari katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya utafiti, wengi walikutwa wameathirika na virusi vya UKIMWI (asilimia 11) ikilinganishwa na asilimia 7 ya wale waliosema walifanya ngono isiyokuwa hatari. Wanawake waliosema hawakufanya ngono katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, walikutwa na kiwango cha juu cha maambukizo ya virusi vya UKIMWI (asilimia 15) ikilinganishwa na waliosema walifanya ngono katika kipindi kama hicho.

Kiwango cha maambukizo kwa wanaume waliosema walifanya ngono na makahaba katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, ni sawa na wale ambao hawakufanya ngono katika kipindi kama hicho.

Wengi wa wanawake na wanaume wenye historia ya kuwa na dalili za magonjwa ya ngono katika kipindi cha mwaka mmoja kabla ya utafiti walikutwa wameathirika ikilinganishwa na wale ambao hawakuwa na dalili zozote za magonjwa ya ngono. Kwa ujumla kati ya wale waliosema walipatwa na dalili za magonjwa ya ngono katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, asilimia 12 wameathirika na virusi vya UKIMWI na kati ya wale ambao hawakupatwa na dalili za magonjwa hayo, asilimia 8 wameathirika na virusi vya UKIMWI.

Asilimia 11 ya wanawake na wanaume waliowahi kupima afya zao walikuwa wamethirika na virusi vya ugonjwa wa UKIMWI ikilinganishwa na asilimia 7 ya wale ambao hawakuwahi kupima afya zao.

Matokeo yanaonesha kwamba, asilimia 79 ya wahojiwa ambao ni waathirika (asilimia 79 ya wanawake na asilimia 80 ya wanaume) hawajui hali za afya zao kama wameathirika au hawajaathirika, aidha kwa sababu hawajawahi kupima au walipima ila hawakupata majibu ya vipimo vyao.

**Kiwango cha Maambukizo ya Virusi vya UKIMWI kwa Vijana wa umri wa miaka 15 – 24**

Maambukizo kwa vijana wa kike ni asilimia 4 na kwa vijana wa kiume ni asilimia 3. Vijana waishio mijini wanaonekana kuathirika zaidi ikilinganishwa na wenzao waishio maeneo ya vijijini. Wasichana walio katika umri huu ambao waliwahi kuishi katika ndoa hapo awali, wameathirika kwa wingi (asilimia 18), ikilinganishwa na asilimia 5 ya wavulana wa umri kama huo ambao hapo awali waliwahi kuishi katika ndoa. Wavulana wa umri huu ambao kwa sasa wanaishi katika ndoa wameathirika kwa wingi (asilimia 5) ikilinganishwa na asilimia 4 ya wasichana wa umri kama huo ambao kwa sasa wanaishi katika ndoa.

Asilimia 2 ya vijana ambao walieleza kwamba hawajawahi kujamiiana, wana maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii inaweza kuhusishwa na njia nyingine za maambukizo ya virusi vya UKIMWI hasa ile ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

**Kiwango cha Maambukizo baina ya wapenzi wanaoishi pamoja**

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba asilimia 90 ya wapenzi wanaoishi pamoja (yaani ambao hawajafunga ndoa ya aina yoyote), hawana maambukizo ya virusi vya UKIMWI, wakati asilimia 3 ya wapenzi hawa (wote wawili) wameambukizwa virusi vya UKIMWI. Pia matokeo yanaonesha kwamba asilimia 8 ya wapenzi hawa, mmoja wao ameambukizwa na mwingine hajaambukizwa virusi vya UKIMWI.

# KIWANGO CHA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI KIMKOA

